# Njoo Nifuate

## Kitabu cha Kujisomea

Toleo la Kwanza la Kiafrika, 2022

**Tim Green**

Come Follow Me

# Shukrani

Napenda kumshukuru kila mmoja aliyesaidia katika mradi huu kwa kunitia moyo, ukosoaji na maombi.

# Maelezo kuhusu toleo hili la kwanza la Kiafrika

Kwa asili niliandika kozi hii kwa ajili ya watu wa mazingira maalumu ya kidini walioishi katika nchi yao, lakini kwa sasa kuna watumiaji wengi tu katika nchi mbalimbali zikiwemo nchi za Magharibi. Mambo ya kimtazamo bado ni muhimu, lakini viongozi wa kozi hii lazima wayapokee maswali ya majadiliano katika muktadha wao.

Hili ni toleo la Kiafrika. Toleo hili hupatikana katika tovuti ya (come-follow-me.org), ambayo pia hutoa taarifa kuhusu tafsiri za lugha mbalimbali. Toleo tofauti kwa ajili ya watu wa Uingereza litatolewa baadaye.

Faida yo yote ipatikanayo kutokana na mauzo ya kozi hii hutumika kuendeleza mradi huu. Tafadhali nitumie maoni yako kwa uboreshaji zaidi wa matoleo yajayo.

Tim Green, Februari 2019: https://come-follow-me.org/contact-us
Walter Eric, Mei 2022: https://life-challenge.org

# Kwa maelezo zaidi

na kupakua Mwongozo wa Mshauri, tembelea tovuti ya

www.come-follow-me.org

# Haki Miliki

Toleo la kwanza la Kiingereza ni mwaka 2013 katika tovuti ya Lulu.com. Haki zote zimehifadhiwa.

Toleo la pili, 2017. © Haki miliki. Tim Green 2013.

Wasomaji wanaruhusiwa kurudufisha hadi masomo mawili ya kitabu hiki cha kujisomea, au kuchapa somo la majaribio kutoka kwenye tovuti yetu, kwa idadi wanayotaka lakini siyo kwa kuuza. Tafadhari usirudufishe zaidi ya masomo mawili. Kwa mawasiliano zaidi, tafadhari wasiliana nami kwa barua pepe comefollowmecourse@gmail.com

**Toleo la Kiswahili**
**© 2022 na Tim Green**
**ISBN: 9789976-70-057-2**

Labda ielezwe vinginevyo, Maandiko yote yametolewa katika The Holy Bible, in Kiswahili, Union Version. Published as MAANDIKA MATAKATIFU. © Bible Society of Tanzania, 1997

*Kimewekwa wakfu kwa ajili ya wote wanaochuchumilia*
*maisha mapya katika Kristo, na kupata sehemu yao*
*katika jumuia yake, huku wakizijali familia zao na jumuia zao za*
*zamani bila kujali hali yao ya kutoeleweka au kukataliwa.*


# Tafadhali soma hapa kwanza!

Kozi hii ya *Njoo Nifuate* ni ya kukusaidia wewe kukua katika Kristo na katika jumuia yake.

Kitabu hiki cha kujisomea siyo kozi kamili! Ni sehemu ya kwanza tu kati ya sehemu tatu. Hivyo fuata utaratibu huu:

- **Kwanza**, kamilisha maswali ya kujisomea binafsi kwa somo moja (ukrasa wa *vi* unaelekeza namna ya kufanya hivyo);
- **Pili**, jadili swali hilo na mshauri wako au katika kikundi;
- **Tatu**, weka katika vitendo sehemu ya 'Tekeleza kwa Vitendo'.

Hatua hizi zimeunganishwa ili kuitaarifu akili yako, kubadilisha moyo wako na kuiwezesha mikono yako kushiriki katika huduma kwa vitendo.




***Hivyo, usisome tu kitabu hiki ukiwa peke yako.*** Badala yake, tafuta mfuasi mzuri wa Kristo akusaidie akiwa kama mshauri wako. Baada ya kila somo la kujisomea binafsi, kutana na mshauri wako. Jadilini pamoja kile unachojifunza na namna ya kutekeleza kwa vitendo. Omba ushauri kutoka kwa mtu huyo kuhusu mambo ya maisha yako. Omba pamoja na mtiane nguvu kila mmoja na mwenzake katika Kristo. Utanufaika zaidi kama utafanya hivyo katika kikundi pamoja na waamini wengine.

Kama wewe ni mshauri unayetumia kozi hii ya *Njoo Nifuate*, tafadhali pata ***Mwongozo wa Mshauri*** ambao unaeleza namna ya kutumia kozi hii.

'Dokezo la kitamaduni' zitakusaidia kuelewa mada na kuna maswali ya majadiliano kwa kina kwa kila somo. Pakua bure Mwongozo wa Mshauri kutoka katika tovuti ya **come-follow-me.org** au wasiliana na shirika la Life Challenge ili uweze kujinunulia nakala yako.

Haijalishi wewe ni mwanafunzi au mshauri, tafadhali tutumie maoni yako. Tupatie maoni yako kwa ajili ya kuboresha na tuambie kama ungependa kujua kuhusu kozi zingine.

Asante sana!

Tim Green comefollowmecourse@gmail.com
Walter Eric info@lifechallenge.de
www.come-follow-me.org

# Yaliyomo


| Somo | | Page |
|---|---|---|
| 1 | **KUFANYIKA MFUASI WA KRISTO** | 1 |
| 2 | **MAISHA MAPYA NDANI YA KRISTO** | 7 |
| 3 | **MUNGU BABA** | 13 |
| 4 | **KUMTII KRISTO KWA NGUVU ZA ROHO WAKE** | 18 |
| 5 | **KUZUNGUMZA NA MUNGU** | 24 |
| 6 | **NENO LA MUNGU KWA AJILI YETU** | 30 |
| 7 | **WASHIRIKI WA KANISA LA KRISTO** | 36 |
| 8 | **WASHIRIKI WA JUMUIA MBILI** | 42 |
| 9 | **SABABU ZA KUTESWA** | 48 |
| 10 | **MWITIKIO KWA MATESO** | 54 |
| 11 | **WAUME NA WAKE** | 60 |
| 12 | **KUTATUA MIZOZO YETU** | 67 |
| 13 | **KUTOA USHUHUDA** | 75 |
| 14 | **UBATIZO** | 82 |
| 15 | **NJIA ILIYONYOOKA** | 88 |
| 16 | **SHERIA YA UPENDO** | 94 |
| 17 | **KUFUNGA NA KUTOA** | 100 |
| 18 | **MAJALIWA NA UCHAWI** | 107 |
| 19 | **KUTUMIKIANA** | 114 |
| 20 | **HIJA YETU KWENDA MBINGUNI** | 121 |
| | Nyongeza ya 1: **Muda Wangu wa Kila Siku na Mungu** | 129 |
| | Nyongeza ya 2: **Namna ya Kumfikia Mungu** | 131 |
| | **Mwongozo wa Majibu** | 135 |

# Mwongozo kwa Mwanafunzi

**1** Karibu kwenye Kosi hii! Itakuwa ni msaada sana kwako kumfuata Bwana Yesu Kristo katika maisha yako ya kila siku. Mimi ni mwalimu wako na huu ni mwongozo wa kukusaidia kunufaika na kozi hii.



**2** Usisome kozi hii ukiwa peke yako – hutafaidika. Tafadhali tafuta mfuasi mzuri wa Kristo ili akusaidie kama mshauri. Baada ya kila juma kuwa umejisomea nyumbani, kutana na mshauri wako ili mjadiliane – na inapendekezwa uwe na mwanafunzi mwenza pia.

**3** Na zaidi ya yote, weka masomo haya katika vitendo katika maisha yako ya kila siku! Kila somo lina “Kazi ya Kufanya” kwa ajili yako kufanya kwa wiki ijayo.

1. . Soma kila swali kwa makini.

2. Andika alama ya vema [√] kwenye jibu lako katika nafasi iliyoachwa wazi katika kila swali.

3. Baada ya kuandika jibu lako, unaweza kulinganisha na majibu yaliyotolewa mwishoni mwa somo hili.

4. Baada ya kukamilisha kila somo, fanya Marudio ya Somo ili kupitia mawazo makuu.

5. Baadhi ya maswali yanakuomba ulete mawazo yako katika kipindi cha majadiliano. Hakikisha unajibu maswali haya na uwe tayari kwa majadiliano.

6. Kwa masomo matano ya kwanza kitabu pekee unachohitaji ni kitabu cha kozi hii tu. Kuanzia somo la 6, utahitaji kuwa na nakala yako ya Biblia Takatifu. Katika kozi hii, tutatumia The Holy Bible in Kiswahili, Unioni Version, Published as Biblia (toleo la 1997), lakini kama una tafsiri nyingine ni sawa tu. Kuna tafsiri nyingi za Biblia, lakini zinatoka kwenye lugha ya asili. Lugha ya asili haibadiliki.

7. Ulimwenguni kote kuna wafuasi wengi sana wa Kristo ambao wanatokana na dini ileile ya kale kama ulivyo wewe. Baadhi yao wana elimu zaidi na wengine siyo. Kozi hii imeandikwa kwa njia iliyo rahisi ili kwamba watu wasio na elimu ya juu wanaweza kuelewa. Unaweza kuona mtindo wa kufundisha ni rahisi sana, lakini utautii katika maisha yako? Mungu anajali utii wako hasa kuliko akili zako. Kama utatii mafundisho, utanufaika sana.

8. Kumbuka, mshauri wako anatoa muda wake ili kukusaidia wewe. Mheshimu mtu huyo kwa kufika kwa muda uliopangwa kwa ajili ya majadiliano, na kwa kukamilisha kazi zako za nyumbani.

***Sasa anza kwa msaada wa Bwana!***

Somo la
# 1 KUFANYIKA MFUASI WA KRISTO



## Kusudi la Maisha Yetu

Watu wawili walikuwa wakijadiliana. Mmoja wao alisema, “Ninaamini kwamba Mungu Mweza wa Yote aliniumba ili nitii sheria zake. Aliwatuma manabii kunionyesha mimi Njia Iliyonyoka. Kama nitaifuata njia hiyo basi natumaini Mungu atanisamehe dhambi zangu na kuniruhusu niingie Paradiso. Hilo ndilo kusudi la maisha yangu.”

Yule mtu wa pili alijibu, “Hata mimi pia nataka kuzitii amri za Mungu. Lakini siogopi kwamba atanipeleka kwenye ziwa la moto. Amekwisha kunisamehe dhambi zangu na ameahidi kunikaribisha mbinguni. Hivyo, hapa duniani ninafurahi kumjua yeye binafsi, ninahisi upendo wake na ninampenda pia. Ninataka niishi kwa ajili yake, kila nukta ya maisha yangu ya kila siku. Hili ndilo kusudi la maisha yangu."

Kufikiria: Je! Unakubaliana na mtu wa kwanza au wa pili? Au una kusudi lingine la maisha yako? Nini kusudi la maisha yako?



**1** Pale tunapofikiria kuhusu maisha yetu inaweza kuwa mzigo kwetu. Tunalemewa na matatizo yetu kwa sasa na mashaka yetu kuhusu mstakabari wetu. Katika Injili Takatifu (Injil) Bwana Yesu Kristo alitoa ahadi ya ajabu ambayo ni kwa ajili yetu:

***“Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.”*** (Matayo 11:28)

Fikiria kwamba Yesu Kristo anasema na wewe binafsi maneno haya! Endelea kuyarudia mpaka uweze kuyasema kwa kukariri. Kisha jaza katika nafasi zilizoachwa wazi hapo chini:

“Njoni kwangu, ninyi nyote____________ na _______________, nami itawapumzisha.”

**2** Bwana Yesu Kristo alizungumza maneno haya alipokuja hapa duniani. Aliwaita watu waje kwake: “njoo, **ni**fuate”. Baadhi yao waliitikia kwa furaha na kufanyika wafuasi wake. Wengine walimkataa. Kristo yu hai leo na bado anatoa mwaliko uo huo kwetu. Mwaliko huu ni upi?

“Njoo,_____________”.

## Kufanyika Mfuasi wa Kristo

**3** Hebu tujifunze namna ya kufanyika mfuasi wa Kristo. Tunaweza kufuata mfano wa mvuvi aliyeitwa jina lake Simoni Petro ambaye alikuwa mmoja wa wafuasi wa Kristo. Hebu tuisome habari hii kutoka katika Biblia Takatifu:

> ***Ikawa makutano walipomsonga wakisikiliza neno la Mungu, yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni. Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni, 'Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki.' Simoni akajibu akamwambia, 'Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu.' Basi walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika…Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema, 'Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana.' Maana alishikwa na mshangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata…Yesu akamwambia Simoni, 'Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu.' Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao, wakaacha vyote wakamfuata."*** (Luka 5:1-11)

Baada ya kuwa umekisoma kifungu hiki, weka alama ya vema (√) kwenye kisanduku hiki ☐ na endelea.

**4** Inaonekana kwamba Simoni Petro alichukua *hatua nne* ili kufanyika mfuasi wa Yesu. Kwa hatua hizo nne watu wa leo wanaweza kuwa wafuasi wa Bwana Yesu. Hebu tujifunze sasa hatua hizo nne.

### Hatua ya Kwanza: Geuka na kuiacha dhambi

Simoni alipouona muujiza wa samaki, macho yake yalifunguliwa. Aliutambua utakatifu wa Bwana Yesu, na kinyume chake akajiona yeye alivyo mwenye dhambi. Alisema nini kwa Yesu? "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni_____________" *(ona kifungu hicho hapo juu, paragrafu ya mwisho)*

**5** Simoni alitambua kwamba yeye alikuwa mtu 'mwenye dhambi'. Yawezekana alikuwa hajaua mtu ye yote, au hajafanya uzinzi. Lakini Yesu anaweza kuona ndani ya moyo. Simoni hakuweza kuficha cho chote mbele ya Yesu, siri za moyoni mwake au mawazo yake mabaya.

Je! Wewe? Siri zako zilizofichika ni zipi, ambazo zinaweza kukufanya ukafadhaika kama zingetangazwa hadharani ndani ya kanisa lenu? Yawezekana unaweza kuzificha siri hizo majirani na familia wasiweze kuzijua, lakini huwezi kumficha Yesu Kristo. Anaweza kuona kila kitu kiovu kilichofichika maishani mwako kwa uwazi kama daktari awezavyo kuona mifupa yote iliyofichika ndani yako kwa kutumia kipimo cha X-ray!

*Pumzika sasa, na mwombe Yesu. Kristo akuonyeshe kona zenye giza maishani mwako*.

**6** Ni kweli, kila mtu amechafuliwa na dhambi. Kama mwanamashairi wa huko Uajemi aitwaye Omar Khayyam (1048-1131) alivyosema,

"Niambie ni nani ambaye hajatenda dhambi hapa duniani
Niambie wako wapi hao ambao hawajatenda dhambi,
Ninakukosea na wewe unanikosea mimi
Hivyo niambie tofauti iliyopo kati yako na mimi."

Je! Mtu anaweza kuficha dhambi yake mbele za Mungu? [Ndiyo / Hapana]
*(zungushia mduara jibu lililo sahihi)*

**7** Hapo mwanzo ulikuwa umefundishwa kwamba Mungu anawapenda wanaojisafisha na anawachukia watenda maovu. Lakini Yesu aliye Msafi kuliko wote alimchukia Simoni kwa kuwa hakuwa safi? Inashangaza, hakufanya hivyo! Yesu alimwambia nini Simoni? (ona kifungu cha swali la 3 na weka alama ya vema kwenye jibu sahihi:)

_ a) ‘Ondoka kwangu’
_ b) ‘Usiogope’

**8** Simoni alijisikia kupumzika moyoni mwake aliposikia Yesu akisema ‘usiogope’! Hata wewe, kama Simoni, unapotambua kwamba u mwenye dhambi, jipe moyo. Yesu ambaye ni Masihi aliyatoa maisha yake kwa ajili yako, kama Nyongeza ya 2 “Namna Ya Kumfikia Mungu” inavyoliweka wazi jambo hili. Yuko tayari kusamehe na kukusafisha kabisa ukawa safi!

Je! Uko tayari kuipokea zawadi yake ya ukarimu? Hebu waone watu hawa wawili wanavyotofautiana:





***Imran*** ***Shafiq***

Yesu Kristo atamsafisha mtu wa aina gani: mtu mwenye kiburi kama Imran au mnyenyekevu kama Shafiq?_______________________________________

**9** Yesu alisema, ‘Sikuja kuwaita wenye haki, *‘bali wenye dhambi, wapate kutubu’ (Luka 5:32).* ‘Toba’ maana yake ni kugeuka nyuma na kuelekea mwelekeo mwingine. Hebu waone watu hawa wawili:

a) Ni nani kati ya watu hawa ametubu, 1. au 2.?
_________

b) Ni yupi ambaye bado anaendelea katika njia yake ya zamani, 1. au 2.? ______________
.



**1.** **2.**

**10** “Kuungama” si tu kusikitikia dhambi dhambi zetu. Inamaanisha kuacha kabisa dhambi, kama alivyofanya yule mtu kwenye picha ya pili. Kwa hivyo, ni ushahidi upi unaonyesha uungamo wa kweli? *(Chagua jibu moja)*

___ a) kujisikia umesikitia maisha yako ambayo yamechafuliwa na dhambi
___ b) kusikitikia dhambi zako bila kubadilisha mwenendo wa Maisha yako
___ c) kuachana kabisa na dhambi na kubadilisha mwenendo wa maisha yako

**11** Ni hatua ipi ya kwanza aliyoichukuwa Simoni ili awe mfuasi wa Yesu? Turn away from__________

## Hatua ya Pili: Kuitambua gharama

**12** Hatua iliyofuata kwa Simoni ilikuwa ni <u>kuitambua gharama</u> ya kufanyika mfuasi wa Kristo. Simoni alikabiliwa na uamuzi mgumu. Yawezekana alikuwa amebanwa na mawazo mawili:




Simoni alitambua nini_____________ya kufanyika mfuasi wa Kristo.

**13** Yesu alisimulia mfano huu kuhusu gharama ya kufanyika mfuasi wake:

> ***"Tena ufalme wa mbinguni umefanana na hazina iliyositirika katika shamba; ambayo mtu alipoiona, aliificha; na kwa furaha yake akaenda akauza alivyo navyo vyote, akalinunua shamba lile."*** (Mathayo 13:44)

Kama mfuasi wa Yesu, ni mambo gani ya gharama kubwa ambayo itabidi uyaache? Weka alama ya vema kwenye jibu sahihi. Unaweza kuchagua jibu zaidi ya moja au zaidi ya haya: *(jibu lako mwenyewe)*

____a) sifa yako katika jamii
____b) ajira au shughuli yako
____c) familia yako
____d) mali yako au urithi wako
____e) mengine *(andika hapa)* ____________________________________

**14** Lakini 'lulu moja ya thamani kubwa' inatosha! Na dhabihu yo yote tuliyoitoa kwa ajili ya Kristo, kumbuka kwamba yeye alishatoa dhabihu kubwa zaidi kwa ajili yetu pale msalabani!

> ***"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwatungali wenye dhambi."*** (Warumi 5:8)

Hivyo, ni nani aliyelipa gharama kubwa: sisi au Kristo? ___________________________

Katika somo la 9 na 10 tutajifunza namna Yesu Kristo anavyotusaidia pale tunapokutana na mateso.

## Hatua ya Tatu: Kujitoa mwenyewe kwa ajili ya Kristo

**15** Kufanyika mfuasi wa Kristo, kwanza, Simoni ilimlazimu aiache dhambi, na pili kuitambua gharama. Kisha aliingia katika hatua ya tatu: "Kujitoa mwenyewe kwa ajili ya Kristo".

Katika namba 3 ya mfululizo huu, soma tena sentensi ya mwisho ya kifungu hicho. Simoni na wenzake walifanya nini kama mwitikio wao kwa wito wa Yesu? *(jaza nafasi iliyoachwa wazi)*

"Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao___________vyote ____________."

**16** Simoni alijitoa mwenyewe kikamilifu kwa bwana wake mpya Yesu.

Ni kwa namna gani tunajitoa wenyewe kwa mtu fulani katika maisha ya kila siku? Hii hapa ni mifano:

- ✓ ***Mtoto aliyechoka*** hujitoa mwenyewe kwa baba yake anapomrukia mikononi mwake ili abebwe.
- ✓ ***Mgonjwa*** hujitoa mwenyewe kwa daktari pale anapokunywa dawa.
- ✓ ***Msafiri*** hujitoa mwenyewe kwa dereva wa gari mwanzoni mwa safari hatarishi.

Kama alivyo mtoto, mgonjwa au msafiri, lazima tujitoe wenyewe kwa ajili ya Yesu pale tunapojiweka mikononi mwa Yesu. Tunajitoa wenyewe maana tunajua anatulinda na kutuongoza. Tunamtii yeye kuwa ni bwana wetu.

Hatua ya tatu ni ipi katika kufanyika mfuasi wa Kristo?

1. Kugeuka kwa kuiacha dhambi
2. Kuitambua gharama
3. ___________mwenyewe kwa ajili ya Kristo

**17** Baada ya kujitoa mwenyewe kwa ajili ya Yesu Kristo, Simoni Petro alisafiri pamoja naye kwa muda wa miaka mitatu. Alishiriki katika furaha na huzuni ya bwana wake. Alimwona Yesu akiponya wagonjwa na kufufua wafu! Alijifunza kuwapenda watu kama Yesu alivyowapenda watu. Polepole mwanafunzi Simoni alimfanana mwalimu wake Yesu. Baadaye alifahamika sana kwa jina lake la pili ambalo ni Petro.

Ni kwa namna gani Simoni Petro alifanyika mfuasi wa Kristo? (*chagua moja*)

_______a) Kwa kujitoa mwenyewe kwa ajili ya Kristo
_______b) Kwa kusema kutoka kichwani imani mpya *(kalima au shahada)*

**18** Kama ujuavyo, mwanafunzi hujifunza kutoka kwa bwana wake kwa kuangalia na kuiga kile anachokifanya. Hiki ndicho Simoni Petro alichokiendeleza akiwa 'mwanafunzi' wa Yesu.

Na sisi pia tunakuwa wanafunzi tunapomfuata Yesu bwana wetu. Ingawa hatuwezi kumwona kwa macho yetu ya nyama, tunajifunza kuiga kile anachokifanya na kufanyika kama yeye. Tuna heshima ya kushiriki katika kazi yake.

Ni ipi hatua ya tatu ya kufanyika mwanafunzi wa Kristo____________mwenyewe kwa ajili ya Kristo.



## Hatua ya Nne: Jiunge na jumuia ya Kristo

**19** Simoni Petro alipotii wito wa Yesu, hakuwa peke yake. Alijiunga na jumuia ya Kristo. Wanafunzi wa Yesu waliishi kwa pamoja kama kundi moja na walishirikiana. Walikuwa wa kabila tofauti na ngazi tofauti za kijamii. Lakini walijifunza kupendana kila mmoja na mwenzake.

Hii haikuwa rahisi. Wakati mwingine walikuwa na hoja. Lakini walimaliza migogoro yao na kusameheana kila mmoja na mwenzake. Simoni Petro alijifunza kwamba wote walio wa Kristo lazima wajiunge na___yake.

***Kujiunga na jumuia ya Kristo ni jambo muhimu kwa kila muumini!***
***Tutajifunza zaidi jambo hili katika somo la 7.***

**20** Yesu Kristo alimwita Simoni Petro kuwa mfuasi wake. Hii inahusisha hatua nne zipi?

1. ________________kwa kuiacha dhambi.
2. ______________________gharama.
3. __________________mwenyewe kwa ajili ya Kristo.
4. ______________________jumuia ya Kristo.



Elezaneni ni ipi kati ya hatua hizi tatu zinakufaa zaidi.



Hatimaye, somo la leo linamaanisha nini kwako binafsi?

- ***Yawezekana tayari wewe ni mfuasi wa Kristo?*** Kama ni hivyo, kozi hii itakusaidia kuendelea kukua katika Kristo.
- ***Yawezekana uko tayari kufanyika mfuasi wa Kristo sasa?*** Basi zungumza na mshauri wako kwa siri, na yeye atakusaidia kuchukua hatua hii.
- ***Yawezekana unahitaji muda zaidi wa kufikiria hatua hii muhimu?*** Ni sawa, lakini usichelewe kufanya uamuzi huo, maana siku moja inaweza kumaanisha umechelewa. Endelea kujisomea kozi hii kama unataka, lakini utanufaika zaidi kama baada ya hapo utachukua uamuzi wa kumfuata Kristo.

**KAZI YA KUFANYA**

*Wiki hii, tafuta mahali ambapo utakuwa peke yako na fikiri kwa makini kuhusu maswali haya.*
Je! Tayari wewe ni mfuasi wa Kristo? Au uko tayari kuwa mfuasi wake? Au unataka muda zaidi wa kufikiria kuhusu uamuzi huu?

Sasa fanya Marudio.

## MARUDIO

1. Ni ukaribisho upi wa ajabu wa Yesu Kristo ulioukariri kutoka katika Mathayo 11:28? *(kama umesahau, ona namba 1 katika mfululizo wa namba hapo juu)*

"Njooni kwangu, ninyi nyote ____________________________________________________
____________________________________________________________(Mathayo 11:28)."

2. Taja hatua nne za kufanyika mfuasi wa Kristo:

1. __________________________________kuiacha__________.
2. ______________________________________________________.
3. ______________________mwenyewe kwa ajili ya___________________.
4. ____________________ya Kristo.

Somo la

# 2 MAISHA MAPYA NDANI YA KRISTO




**1** Hebu tujifunze kuhusu maisha haya mapya na ya ajabu kutoka katika sehemu ya Biblia Takatifu iitwayo 'Waraka wa Kwanza wa Petro', au kwa kifupi ni 1 Petro. Simoni Petro, ambaye tulijifunza habari zake katika somo la 1, aliandika waraka huu chini ya uongozi wa Mungu. Waraka huu huanza namna hii:

***"Petro, mtume wa Yesu Kristo."*** (1 Petro 1:1)

Cheo gani alichonacho Petro mahali hapa? (*chagua moja*)

____a) mwanafunzi ____b) mtume ____c) nabii

**2** Katika Biblia Takatifu, neno 'mtume' maana yake ni mtu aliyetumwa kwa jukumu maalumu (siyo mtu ambaye kitabu kitakatifu kilimshukia). Yesu Kristo alichagua wanaume kumi na wawili, aliwafundisha na aliwatuma kwa jukumu maalumu. Ndiyo maana wanaitwa 'mitume'. Kiongozi wao alikuwa mtume Petro.

Ni sehemu gani ya Neno la Mungu tutakayoisoma katika kozi hii? Waraka wa kwanza wa mtume _______

**3** Mstari wa kwanza wa 1 Petro unatuambia ni nani aliyeandika waraka huu chini ya uongozi wa Mungu. Pia inatueleza aliyeupokea waraka huu. Walikuwa wafuasi wa Kristo katika nchi ambayo sasa inaitwa Uturuki. Katika mstari huu wanaitwa "wateule wa utawanyiko".

***Tulia kidogo na mshukuru Mungu kwa kutufanya sisi kuwa wateule wake!***

**4** Mstari uleule unawaita "wakaao hali ya ugeni". Yawezekana unaishi mbali na nchi yako ya nyumbani. Au bado unaishi katika nchi yako, lakini umejitenga na familia yako kwa sababu wamekukataa. Huu ni uzoefu mgumu sana!

Lakini katika macho ya Mungu, ni utambulisho gani mpya tulio nao? Sisi ni___________a Mungu'

## A) Utambulisho wetu mpya

**5** Ndiyo, sisi ni 'wateule wa Mungu'! Jumuia yetu ya kwanza inaweza kutukataa, lakini *"Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?... Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu?"* (Warumi 8:31,33). *"Na Mungu, je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku…?"* (Luka 18:7)

Tukiwa wafuasi wa Kristo, utambuisho wetu mpya ni nini? (*chagua moja*)

_____a) wateule wa Mungu_b) najisi______c) wakengeufu

**6** Mstari unaofuata unasema *"kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua"* (1 Petro 1:2)


Kuna habari inayosimuliwa kuhusu kijana aliyepoteza wazazi wake wa kumzaa. Walezi wengine walimlea mpaka akakua na kumwasili kuwa mtoto wao. Siku moja watoto wenzake walianza kumtania kuhusu jambo hilo. Alijibu, "Hapana, najisikia kuheshimiwa zaidi kuliko ninyi. Baba zenu hawakuwachagua lakini baba yangu alinichagua kuwa mtoto wake.

Ni heshima iliyoje kuwa mteule wa Mungu! Je! Tulistahili kutokana na matendo yetu mema? [Ndiyo/Hapana ]

**7** Mungu alituchagua kwa sababu anatupenda, siyo kwamba tunastahili. Pia ni kweli kwamba tulichagua kumfuata Mungu kupitia kwa huyu Yesu Kristo. Wakati mwingine uchaguzi wa Mungu na wetu hufanyakazi kwa pamoja.

Utambulisho wetu mpya katika Kristo ni nini? Sisi ni____________wa Mungu.

## B) Uzao wetu Mpya



**8** Unaijua tofauti kati ya mnyoo na kiwavi. Ingawa wanaonekana kufanana, lakini kuna tofauti kubwa sana kati yao. Mnyoo hutambaa bila kuwa na mabadiliko yo yote mpaka unakufa. Lakini kiwavi hupitia mabadiliko ya ajabu. Badala ya kufa, hufanyika nini? *(ona picha)*

____________________

**9** Je! Si maajabu hayo kwamba kiwavi ambavyo kilikuwa kikitambaa kwenye jani la mti, kimebadilika na kuwa kipepeo mzuri ambaye anapaa angani? Ni sawa na kupita katika 'uzao mpya' ili kuwa kiumbe kipya.

Ni mabadiliko gani hutokea kwa kiwavi? Aina ya '____________mpya'

**10** Je! Umefanyika mfuasi wa Yesu Kristo? Ukitazama kwenye kioo, kwa mwonekano wa nje utaona mtu yule yule kama ulivyokuwa zamani. Lakini kwa kweli, mabadiliko ya ndani yako ni makubwa kama kiwavi anavyofanyika kuwa kipepeo. Mabadiliko haya ya ajabu huitwa 'uzao mpya'.

Ni watu gani wanaopata uzoefu wa uzao huu mpya? (*chagua moja*)

____a) watu wote wakaao katika nchi yetu
____b) ni wale wote waliojitoa wenyewe kwa ajili ya Kristo
____c) watu wote waliozaliwa katika familia za Kikristo

**11** Mstari unaofuata wa 1 Petro unatueleza kuhusu uzao huu mpya:

> ***"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu"*** (1 Petro 1:3)


Kutokana na mstari huu, ni nani aliyetupatia uzao huu mpya?

____a) **Mungu**, kwa rehema zake nyingi
____b) **sisi**, kwa matendo yetu
____c) **mtu mtakatifu**, kwa sala zake kwa ajili yetu

## Je! Umekwisha kupata uzoefu huu wa uzao mpya?

**12** Mungu hutoa uzao huu mpya kwa kila mmoja, lakini siyo kila mmoja huupokea.


Ona daktari anavyowaambia wagonjwa hao watatu, na majibu yao:




Ni mgonjwa yupi kati ya hawa, A. B. au C. atakayepona? __________

**13** Kwa namna ileile, ni yupi kati ya watu hao watatu hapo chini atapokea uzao mpya katika Kristo? (*chagua moja*)

_a) Yule asemaye, “Naamini mafundisho yako, Kristo, lakini naogopa kukupokea maishani mwangu”
b) Yule asemaye, “Sikuamini”
c) Yule asemaye, “Nakuamini, Bwana Yesu. Sasa nakupa maisha yangu. Tafadhali ingia maishani mwangu”.




## C) Asili yetu mpya

**14** Tumejifunza kuhusu ‘utambulisho wetu mpya’ na ‘uzao wetu mpya’ kama wafuasi wa Kristo. Pia Yesu Kristo hutupatia ‘asili mpya’, ambayo ni asili yake ndani yetu.

Watu wengi wenye dini zao za zamani wamefanyika wafuasi wa Kristo. Baadhi yao ni hawa hawa wakieleza mabadiliko chanya yaliyotokea katika maisha yao: *(majina mbadala yametumika)*

| | |
|---|---|
| ***Talib:*** | “Maisha ndani ya Kristo ni ya furaha na kuridhisha moyo” |
| ***Hassan:*** | “Yesu alinipa furaha na amani” |
| ***Said:*** | “Mashaka na wasiwasi wangu vilitoweka” |

| | |
|---|---|
| ***Shaheeda:*** | "Mizigo na hofu yangu vimetoweka" |
| ***Fatuma:*** | "Ninafahamu Mungu hunipokea kama nilivyo" |
| ***Ahmad:*** | "Rangi ya maisha yangu ya kale ilikuwa nyeusi na ilikuwa na harufu ya pombe, wanawake na dhambi. Rangi yangu ya sasa ni mwanga, iliyofunikwa furaha na amani" *(kutoka katika 'Jesus More than a Prophet' na Ralph Wotton)* |

Wote hawa ni watu halisi. Ni tofauti zipi zilizoingia maishani mwao? (*chagua moja*)

____ a)Yesu Kristo aliwapa asili mpya pamoja na mabadiliko chanya mengi
____b) Maisha yao yaliharibika zaidi kuliko hapo awali
____c) Hawakubadilika katika asili yao ya kale

**15** Yesu Kristo huwapa asili mpya wafuasi wake wote. Kama wao, sisi pia tutapata uzoefu wa hisia mpya za furaha na amani. Lakini hisia zetu siyo jambo la muhimu sana. Kilicho cha muhimu ni mabadiliko yaletwayo na Yesu katika tabia zetu. Hii hapa ni baadhi ya mifano hai: *(majina mbadala yametumika)*

| | |
|---|---|
| ***Hassan:*** | "Yesu aliniwezesha kuachana na tabia yangu ya uvutaji sigara" |
| ***Jamal:*** | "Yesu alibadilisha nia yangu ya kale iliyojaa kiburi" |
| ***Razzaq:*** | "Hali yangu ya kusitasita na kujisikia mnyonge ilitoweka" |
| ***Said:*** | "Niliacha kuwa mchokozi" |
| ***Shamim:*** | "Nilianza kuwapenda watu wengine" |
| ***Faisal:*** | "Roho ya huduma imechukua nafasi ya kiburi na udanganyifu maishani mwangu" |
| ***Rashid:*** | "Nilijifunza kumtegemea Bwana katika shughuli zangu na kutenda kwa uaminifu" |
| ***Mariam:*** | "Natamani kuwaleta wengine ili walijue pendo la Kristo" |

*(kutoka katika 'Jesus More than a Prophet' na Ralph Wotton)*

Ni mabadiliko yapi Kristo aliyoyaleta maishani mwako? Andika mawazo yako, na uwe tayari kuwashirikisha wengine wakati wa kipindi cha majadiliano:

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**16** Kama bado hujapata uzoefu wa yote hayo hapo juu, usihofu. Utakuja polepole kadiri unavyokua katika Kristo. Huchukua miaka mingi kwa mtoto kukua kuwa mtu mzima, na ndivyo inavyochukua miaka mingi baada ya kupokea 'uzao mpya' ili kukomaa kiroho.

Lakini kwa sababu Kristo anaishi ndani yako, ni 'asili' ipi inayotakiwa kuonekana zaidi ndani yako?

____a) asili yako ya kale yenye dhambi_____b) asili yako mpya ndani ya Kristo

## Vita vyetu vya Kiroho

**17** Ingawa tayari tunayo asili mpya katika Kristo, pia lazima tupigane aina fulani ya vita vya kiroho dhidi ya asili yetu ya kale – kila siku wakati wote wa maisha yetu! Neno la Mungu linatupa amri hii:

***"Basi vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi, vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu [asili] mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba."***
(Wakolosai 3:5,7-10)

Kutokana na mistari hiyo hapo juu, (chora mduara kwenye majibu sahihi)

a) ni asili gani 'tuliyoivua'? [asili ya kale / asili mpya]

b) ni asili gani 'tuliyoivaa'? [asili ya kale / asili mpya]

Jadili jinsi imekuwa vigumu kwako kuvua asili ya kale na kuvaa asili mpya. Eleza mapambano yako.

**18** Picha hiyo hapo chini huonyesha wafuasi wa Kristo wakifanya mambo mbalimbali. Katika nafasi iliyoachwa wazi kwa kila jina, andika 'ya kale' kama mtu anaonyesha tabia ya asili ya kale, au 'mpya' kwa ajili ya asili mpya:




Mtu a): Asili______ Mtu b): Asili______ Mtu c): Asili______ Mtu d): Asili______

**19** Kila siku asili yetu mpya, ambayo ni asili ya Yesu iliyowekwa ndani yetu, hupigana vita dhidi ya asili yetu ya kale yenye dhambi. Mkulima mmoja aliielezea hali hii kama ifuatavyo: "Ninahisi kama vile mbuzi wawili wanapigana ndani yangu, mbuzi mweusi na mweupe." Wasikilizaji wake walimwuliza, "Hivyo ni mbuzi gani aliyeshinda?" Alijibu, "Yule niliyemlisha zaidi!"

***Fikiria mfano huu wa mkulima. Mbuzi mweusi anawakilisha asili yetu ya kale na yule mbuzi mweupe anawakilisha asili yetu mpya. Ni yupi anayeshinda katika maisha yako siku hizi? Kwa nini? Uwe tayari kwa ajili ya majadiliano.***



Kutokana na somo la leo, hebu tukumbuke faida tatu tulizo nazo katika Kristo:

- Tuna <u>utambulisho mpya</u> kama watu waliochaguliwa na Mungu
- Tumepita katika <u>uzao mpya</u>, kama vile kiwavi kufanyika kipepeo
- Kwa msaada wa Kristo, <u>asili yetu mpya</u> huibadilisha asili yetu ya zamani polepole

**20** Mstari huu kutoka katika Neno la Mungu unatoa muhtasari wa yote tuliyojifunza leo:


> ***"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya!"*** (2 Wakorintho 5:17)

Jaza nafasi zilizoachwa wazi katika mstari huu mpaka uuelewe ndani ya moyo:
"Hata imekuwa ______________________________________________ , amekuwa ___________

kipya; ya kale yamepita ____________yamekuwa mapya!" (2 Wakorintho 5:17)

Sasa sema sala hii:

> "Ee Bwana,
> Kwa rehema zako nyingi umetuchagua kuwa wateule wako – asante sana!
>
> Asante kwa kunipa uzao mpya na asili mpya. Kwa nguvu ya Kristo, nisaidie kila siku kupigana vita vya kiroho dhidi ya asili ya kale yenye dhambi. Amina."



**KAZI YA KUFANYA**

Andaa orodha ya mabadiliko chanya matatu katika maisha yako, ambayo yanatokana na asili yako mpya. Mshukuru Mungu kwa mabadiliko haya. Pia orodhesha tabia tatu kutoka katika asili ya kale ambazo bado zinaonekana katika maisha yako. Kwa wiki hii, kwa msaada wa Mungu, pigana vita dhidi ya tabia hizo mbaya.

## MARUDIO

1 a) Mtu anapojitoa mwenyewe kwa ajili ya Kristo, ni mabadiliko gani hutokea ndani yake?________mpya

b) Ni utambulisho gani mpya tulio nao kama wafuasi wa Kristo? Sisi ni ___________________ _____________wa Mungu

2 Vita vyetu vya kiroho ni dhidi ya asili [ya kale/mpya] ya dhambi na asili [ya kale/mpya] katika Kristo (kata jibu lisilo sahihi)

3 Toa mabadiliko mawili ambayo Yesu Kristo huyaleta ndani ya maisha ya wafuasi wake (kama *huwezi kuwaza hata moja, ona swali la 11-12):* _________________

_______________________________________________________________

4 Jaza kutoka kichwani nafasi zilizoachwa wazi za mstari wa 2 Wakorintho 5:17:

"Hata imekuwa _________ , amekuwa _____ kipya; yamepita _____ yamekuwa mapya!" (2 Wakorintho 5:17)

# WONGOZO WA MAJIBU

## SOMO LA 1 MAJIBU

1 msumbukao, kulemewa
2 nifuate
3 soma kifungu
4 mtu mwenye dhambi
5 jibu binafsi
6 Hapana
7 b)
8 mtu mnyenyekevu
9 a) mtu wa 2; b) mtu wa 1
10 c)
11 dhambi
12 gharama
13 jibu binafsi
14 Kristo
15 wakaacha, wakamfuata
16 kujitoa
17 a)
18 kujitoa
19 jumuiya
20 1.geuka,;2. Kuitambua gharama;
3. kujitoa, Kristo;
4. Jiunge na jumuia




## SOMO LA 2 MAJIBU

1 b)
2 Petro
3 jibu binafsi
4 watu
5 a)
6 Hapana (lakini kama huna uhakika na hili, mshirikishe mshauri wako)
7 wateule
8 kipepeo
9 uzao
10 b)
11 a)
12 11 c)
13 c)
14 a)
15 uwe tayari kwa majadiliano
16 b)
17 a) asili ya kale b) asili mpya
18 a) mpya b) mpya
c) ya kale d) ya kale
19 uwe tayari kwa majadiliano
20 kariri aya

